

Hati ya Urathi na Wasiya wa Ki-Islamu

Imetayarishwa na: Quran and Sunnah Society of East Africa (QSSea) – www.qssea.net

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwenye
Kurehemu

Hati ya Urathi na Wasiya wa Ki-Islamu

Mwusia	
Jina ¹	
Tarehe ya kuzaliwa	
Mji wa Makao	
Wilaya	
Jimbo au Mkoa	
Nchi	

Mimi, _____, nikiwa na akili pamoja na fahamu zangu timamu, ninabatilisha hapa nilipo, kila aina na hati ya wasiya na marekebisho yaliyotangulia, na natangaza yakuwa huu ndiwo wasiya na hati yangu ya urathi wa mwisho.

Dibaji

Shahada – Ubainifu wa Imani

أَشْهَدُ أَنَّ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ، وَأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّداً رَسُولَ اللَّهِ

Ash-hadu allaa ilaaha illallaah, wa ash-hadu anna Muhammadaan rasoolullaah.

Nashuhudia mimi yakwamba hapana Mola wa kweli anaestahiki kuabudiwa kwa Haki isipokuwa Allaah, na kwamba Muhammad (*Sallallaahu ‘alayhi wasallam*) ni Mtume wa Mwenyezi Mungu.

Mimi nashuhudia yakwamba Mwenyezi Mungu ndie muumba wa mbingu na ardhi, Nae ndie Mola wa Aadam, Nuh, Ibraahim, Musa, na ‘Eesa. Nashuhudia yakwamba ahadi za Mwenyezi Mungu ni za kweli na wala hapana shaka yakwamba tutakutana nae,

¹ Mtambulische mwusia kwa uthibitisho usiokuwa na matata ya aina yoyote kwenye Hati, kuanzia mwanzo hadi mwisho. Tumia jina la kawaida linalotumika katika vitambulisho halali.

Pepo ni Haki (kweli), siku ya kuhukumiwa inakuja bila ya shaka yoyote, na kwa hakika Mwenyezi Mungu (Subhaanahu wata'aalah) Atawafufua walioko makaburini mwao.

Usiya kwa Niwapendao

Ufuatao ni Usiya wangu kwa mke wangu, wanangu, jamaa zangu, marafiki zangu, ndugu zangu waislamu waume na wake, na wote watakaoishi baada ya kufa kwangu:

- Fanyeni juhudili muwe ni waislamu wa kweli. Muabuduni Muumba wetu (*Subhaanahu wata'aalah*) kwani Yeye ndiye Anaestahiki kuabudiwa kwa Haki Pekeyake pasi na kushirikishwa na chochote. Elekezeni Uchaji wenu, matumaini yenu, mapenzi yenu, na unyenyekevu wenu kwake Yeye Pekeyake. Nawausia nyinyi kwa yale ambayo Ibraahim na Ya'qoob waliiyowausia nayo watoto wao:

وَصَّىٰ بِهَاٰ إِبْرَاهِيمَ بَنِيهِ وَيَعْقُوبَ يَدْبَنِي إِنَّ اللَّهَ أَصْطَفَنِي لَكُمُ الَّذِينَ

فَلَا تَمُوتُنَّ إِلَّا وَأَنْتُمْ مُسْلِمُونَ 

132. Na Ibrahim akawausia wanawe, na pia Yaaqub: Enyi wanangu!

Hakika Mwenyezi Mungu amekuteulieni Dini hii; basi msife ila nanyi mmekuwa Waislamu, wanyenyeketu.²

- Mnyenyekeni Mwenyezi Mungu na mujisalimishe na amri zake. Na muwe tayari kwa safari ya kuondoka kwenye maisha haya ya kilimwengu. Chukuweni zawadi zenu za amali njema. Fanyeni usuhuba na wanavyuoni na waislamu wema. Ifanyeni miondoko yenu pamoja na maumbile yenu ionyeshe Kifungu cha iliyo bora ya Uislamu. Muwe na juhudili kulingania na kiustawisha Dini ya Uislamu.
- Mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume wake (*Sallallaahu 'alayhi wasallam*). Shikamaneni Imara na Sunnah (mafundisho) za Mtume, na uongofu wa Salaf (waislamu wema wa mwanzo). Nawausia na usiya wa mwisho wa Mtume Muhammad (*Sallallaahu 'alayhi wasallam*) kwa wafuasi wake: <as-Swalaah ... as-Swalaah ...>³. Kwahivyo, simamisheni swala katika nyakati zake zilizowekwa.
- Musiache kuniombea Mungu na mumuombe Allaah (*Subhaanahu wata'aalah*) anighufirie madhambi yangu na Anirehemu.
- Jiepusheni na kila aina ya vitendo viovu. Jitahadharini na mambo ya kuzuwa au kubadilisha chochote katika mafundisho ya Uislamu. Mimi niko kando mbele ya Mwenyezi Mungu na kila aina ya vitendo viovu au vitendo vya uzushi ambavyo mtu yoyote atakaenzua baada ya kufa kwangu.

Mambo ya kufanywa wakati wa mauti

² Al-Baqarah 2:132

³ Imepokewa na Imaam Ahmad na wengineo kutoka kwa Umm Salamat, Anas, na Ibn 'Umar (Radhiyallahu 'anhuma). Imesahihishwa na Sheikh al-Albaani (*Saheeh ul Jaami'*) no. 3873

- (1) Mauti yatakaponihudhuria mimi, nitafutieni Waislamu wema na wenye ilimu wawepo karibu yangu, na wasiache kunikumbusha kudumisha fikra njema kuhusu Mola wangu, ili nitarajie Rehma Zake na msamaha kutoka Kwake na huku wanihimize ili ulimi wangu mara kwa mara uwe unatamka *Shahadah*.
- (2) Ondosheni kwenye hadhara yangu kitu chochote chenye kuwafukuza Malaika wa Rehma, kama vile picha, sanamu za watu au wanyama, mbwa, kengele, wanawake ambao hawakujisitiri kulingana na Sheriya, nyimbo (au miziki), uvutaji sigara, n.k (*na kadhaalika*).
- (3) Baada ya roho yangu kutoweka, mimi naamuru yafuatayo kwa jamaa zangu na wale waliohudhuria:
 - Yafumbeni macho yangu.
 - Niombeeni Du'a njema (bila ya kupaaaza sauti zao), za kunitakia Rehma na Msamaha.
 - Jishughulisheni na kunitayarishia mazishi yangu kwa haraka.
 - Jiepusheni na kutangaza kifo changu kwenye vipaza sauti au magazeti.
 - Wacheni kunikokoteza kutamka *Shahaadah* baada ya roho yangu ikisha toweka kutoka kwenye mwili wangu.
 - Harakisheni kunilipia madeni yangu.
- (4) Hapana mtu yoyote atakae kufa kabla ya wakati wake kufika. Kwahivyo, nawaamuru jamaa zangu yafuatayo:
 - Musijitweke nafsi zenu kwa mauti yangu, lakini badala yake fanyeni matayarisho halisi yenu nyinyi wenywewe.
 - Dumisheni subira, utulivu katika nafsi zenu, najisalimisheni na Qadar ya Mwenyezi Mungu
 - Musipaaze sauti zenu, musiomboleze kwa vilio, musijinyafure nyuso zenu, au musinadi kwa ulinganizi wa *ki-jaahiliyyah* wenyewe kuonyesha kutoridhika kwenu na Qadar ya Mwenyezi Mungu.
 - Wanawake wasiomboleze⁴ kwa kifo changu kwa zaidi ya siku tatu, isipokuwa kwa mjane ambae anaeruhusiwa kuomboleza kwa kufiwa na mumewe kwa muda wa miezi minne na siku kumi – mpaka '*iddah*'⁵ yake ikamilike.

Mazishi

- (5) Mimi naamuru yakwamba mipangilio yangu yote ya mauti na mazishi na yatekelezwe kikamilifu na Waislamu kulingana na Shariya za dini ya ki-Islamu na Sunnah za Mtume Muhammad (*Sallallaahu 'alayhi wasallam*). Si ruhusa kutekeleza shughuli au maandalizi yoyote yasiyoafikiana na Uislamu kwenye mazishi yangu, au kwenye mwili wangu.

⁴ Kuomboleza ni kudhihirisha msiba kwa njia ya kujepusha na kawaida za kuonekana na furaha na anasa.

⁵ Muda wa kusubiri (kukaa bila ya kuolewa) kabla ya kujamulia kuolewa tena.

Hususan:

- Siruhusu upasuaji au kutia dawa ili maiti yangu isioze – isipokuwa kama ikilazimika kutokana na kanuni za ki-Sheriya za nchi.
- Mazishi yangu yasicheleweshwe kutokana na sababu zisizoambatana na muafaka wa Sheriya ya ki-Islamu, kama vile kungoja siku Fulani, au kuwasili mtu Fulani.
- Mwili wangu uoshwe mara tatu au tano (au zaidi ikihitajika) kwa sabuni na maji, pamoja na kafuri au manukato wakati wa mwisho.
- Mwili wangu kitatiliwe ndani ya vitambara vitatu vyeupe safi vilivyo-nyunyiziwa manukato, visiwe na mapambo yoyote wala kitu chochote.
- Nizikwe mahali ambapo nitakapokufa; wala mwili wangu kisisafirishwe zaidi ya umbali wowote usiokuwa na sababu isipokuwa ukihitajika kuwasilishwa kwenye makaburi yaliyokaribu ya Waislamu.
- Mazishi yangu yaharakishwe.
- Mazishi yangu yasiandamwe na wanawake wala vyetezo
- Wakati wa mazishi yangu, sauti zisipaazwe (zisinyanyuliwe) kwa *kusomwa Qur'aan, kupiga Shahaadah*, au maombi yoyote. Utulivu udumishwe hapo, na wale watakaohudhuria wazingatie na kutafakari kuhusu matukio hayo (ya kifo) na huku wakiniombea mimi Mungu ndani ya nyoyo zao.
- Swala nitakayoswaliwa ya maiti itekelezwe nje ya makaburini, na wala si kwenye makaburi.
- Idadi kubwa ya Waislamu wakaribishwe kuja kuswalia maiti yangu, wapangwe mistari mitatu kwa uchache, na waelezwe yakwamba waniombee mimi Mwenyezi Mungu kwa wingi na kwa *Ikhlaas*.

Maziko na Kaburi

(6) Mimi naamrisha yakwamba:

- Kaburi langu na lichimbwe kulingana na vipimo vya Sunnah.
- Ikiwezekana, Kaburi langu lichimbwe mfano wa *lahd*.⁶
- Mwili wangu uzikwe bila ya jeneza au aina yoyote nyengine ya sanduku lenye kutenganisha baina ya mwili wangu uliotatiliwa na mazingara ya udongo. Katika matukio ya sheriya za nchi zenye kulazimu kuzikwa na masanduku, mimi naamuru yakwamba sanduku hilo liwe la sitara na lenye gharama ya chini badala ya sanduku la fakhri.
- Mwili wangu na ulazwe kwenye *lahd* katika upande wa kulia; ukiwa uso wangu umeelekezwa *Qiblah* na mgongo wangu ukihimiliwa na mawe.
- Watu watakaoulaza mwili wangu na waseme; *Bismillaah, wa'alaa millati Rasoolillaah* (kwa jina na Mwenyezi Mungu, na juu ya Dini ya mtume wa Mwenyezi Mungu (*sallallaahu 'alayhi wasallam*)).
- Pasiwekwe mto (wa kulalia) chini ya kichwa changu, pasinyunyizwe manukato yoyote, pasiwekwe mapambo ya aina yoyote katika kaburi langu na

⁶ Sehemu ya chini ya kaburi, kwenye ukuta unaoelekea *Qiblah*, kishubaka kilicholala kwa urefu kichimbwe kiasi cha kutoshea kuingizwa kiwiliwili.

wala pasizikwe pamoja na mimi, kitu chochote kinachohusiana na mapambo ya kidunia.

- Kila atakaehudhuria mazishi yangu na arushe kwa mikono yake, miteko mitatu ya michanga katika kaburi langu kwenye sehemu ya pambizoni mwa kichwa.
- Baada ya kumaliza maziko yangu, waislamu na wasisitizwe ili wasubiri pambizoni mwa kaburi langu kwa muda wa kiasi cha dakika kumi na tano wakiniombea mimi Mwenyezi Mungu bila ya kupaza sauti zao (*kimya*), huku wakiniombea Mwenyezi Mungu Anirehemu, Anighufirie, na Anipe Qauli iliyio *thaabit* nitakapoulizwa na Malaika ndani ya kaburi.

(7) Mimi naamuru yakwamba:

- Pasiezekwe jengo la aina yoyote juu ya kaburi langu.
- Kijunju cha udongo ulioko juu ya kaburi langu usizidi msamba moja wa mkono.
- Kaburi langu lisijengewe boma la aina yoyote.
- Kaburi langu lisiwekewe maandishi wala michoro ya ishara ya aina yoyote, isipokuwa likiwa ni jiwe la kawaida au mchoro wa jina langu ili uwe ni alama ambayo pengine baadhi ya jamaa zangu huwenda wakazikwa mahali hapo.

Kukhalifu amri za Uislamu

(8) Mimi naamuru yakwamba mambo ya uzushi, uvunjaji wa sheria za Uislamu, na vitendo vya wasiokuwa Waislamu ni lazima viepukwe kwenye mazishi yangu.

Hususan:

- Mtu asivae mavazi meusi matupu kama alama ya kuashiria huzuni.
- Mambo yafuatayo yasiruhusiwe katika kuyashughulikia mazishi yangu wala yasiwekwe kwenye kaburi langu; upigaji wa picha, mapambo, mauwa, mauwa yaliyosokotwa kama mnyororo, bendera, au alama za kuashiria kitu chochote.
- Nisisomewe *Qur'aan* (hata kama ni *Soorah al-Faatihah* au *Yaasin*) juu ya mwili wangu wakati wa mazishi yangu.

Tanzia

(9) Mimi naamuru yakwamba:

- Watu waamrishwe jinsi ya kutoa tanzia zao kulingana na muafaka wa *kisheria* wa ki-Islamu uliowekwa.
- Jamaa zangu hawatowahudumikia watu watakaokuja kuwapa pole kwa kuwapa chakula, wala hawatowaajiri au kuamrisha watu kusoma Qur'aan kwa ajili ya matukio hayo.
- Pasiwekwe matanga hususan kwa ajili ya kupokea tanzia, haswa zile zenye kufanywa katika siku za Ijumaa, siku ya tatu, baada ya wiki moja, siku arubaini, kila mwaka, n.k (*na kadhaalika*).

Hati ya Urathi na Wasiya wa Ki-Islamu

Imetayarishwa na: Quran and Sunnah Society of East Africa (QSSea) – www.qssea.net

Mimi najiepusha mbele ya Mwenyezi Mungu, Aliyetukuka, na jambo lolote au maneno yoyote yanayokwenda kinyume na *Sunnah* za Mtume Muhammad (*Sallallaahu 'alayhi wasallam*).

Na hatimae, nawaomba jamaa zangu wote, marafiki na watu wote wengineo, iwapo watachagua kuamini kama nilivyoamini mimi au wasichague hivyo, waiheshimu haki yangu katika itikadi hii. Nawaomba waiheshimu stakabadhi hii, bila ya kuipinga au kuibadilisha kwa njia yoyote. Bali, wacha wajionee wenyewe yakwamba nimezikwa kama nilivyoeleza katika yaliyopita, na wacha mali yangu igawanywe kama nilivyoeleza hapo chini.

KIFUNGU CHA 1 – MATAYRISHO YA MAITI NA MAZISHI

- (1) Mimi hapa, namsimamisha na kumchagua mmojawapo wa wafuatao, kulingana na utaratibu huu, kama ilivyonukuliwa kwa khiyari zao na kuwepo kwao, kuyatekeleza maafikiano yote yaliyo muhimu na yaliyokwisha kuandikwa kwa matayarisho ya mazishi yangu ya *ki-Islamu* kwa njia iliyo sawa.

MSIMAMIZI WA MAZISHI YANGU

	Chaguo La Kwanza	Chaguo La Pili	Chaguo La Tatu
JINA			Imaam Muislamu aliye karibu
ANWANI			
SIMU			

- (2) Katika hali ya utatanishi kwenye usimamizi wa mazishi yangu, namuamuru msimamizi wangu atafute ushauri kutoka kwa Muislamu mwanamume aliye na Ilimu ya kisawasawa au chama cha *ki-Islamu* kinachosifiwa kwa wema.

KIFUNGU CHA 11 – WAKILI NA MLINZI

- (1) Mimi hapa, namsimamisha na kumchagua mmojawapo wa wafuatao, kulingana na utaratibu huu, kama ilivyonukuliwa kwa khiyari zao na kuwepo kwao, awe ndiye wakili wangu wa pekee wa hati hii ya Urathi na Wasiya.

WAKILI WA HATI⁷

⁷ Imependekezwa yakwamba Wakili awe ni kijana wa *Ki-Islamu* mwenye msimamo mzuri wa kidini. Mtu anaweza kumchagua mumewe/mkewe, mwanae, au rafiki.

Hati ya Urathi na Wasiya wa Ki-Islamu

Imetayarishwa na: Quran and Sunnah Society of East Africa (QSSea) – www.qssea.net

	Chaguo La Kwanza	Chaguo La Pili	Chaguo La Tatu
JINA			Imaam Muislamu aliye karibu
ANWANI			
SIMU			

- (2) Namuidhinisha wakili wangu, aliyetajwa hapo juu, uwezo wa kusuluhiha madai yoyote ya mali yangu ninayodai au kudaiwa, na uwezo wa kuuza chochote ninachomiliki, shamba, nyumba, kitu changu binafsi au cha ushirika, chenye kuniletea faida.
- (3) Mimi naamuru yakwamba hapana malipo wala dhamana yoyote ya malipo itakayofungamana na yatakayohitajika na wakili wangu katika utekelezaji wa shughuli zake.
- (4) Ni mapendekezo yangu yakwamba pasiwe na hatua zozote zitakazosikilizwa kwenye mahakama kuhusiana na usimamizi wa mali yangu zaidi ya kuithibitisha na kuihifadhi hati hii, na kisha kuirudisha orodha ya hesabu na kisio la thamani la mali yangu na stakabadhi ya madai yangu.
- (5) Mimi hapa, namsimamisha na kumchagua mmojawapo wa wafuatao, kulingana na utaratibu huu, kama ilivyonukuliwa kwa khiyari zao na kuwepo kwao, na maadamu mtu mwenyewe ataendelea kuwa ni Muislamu muadilifu na mwenye msimamo mzuri wa dini na mtu aliye na busara na akili timamu, awe ni msimamizi wa wahusika na mali wakiwemo watoto wangu kwa vile wao watakuwa ni watoto wadogo wakati na baada ya kufa kwangu, wakiwa kwenye hali yao ya ujana:

MLINZI

	Chaguo La Kwanza	Chaguo La Pili	Chaguo La Tatu
JINA			Imaam Muislamu aliye karibu
ANWANI			
SIMU			

KIFUNGU CHA 111 – MALI ZANGU NA MADARAKA

- (1) Mimi namiliki au nadaiwa thamani ya pesa na bidhaa, madeni,dhamana, biashara, mali, Bank accounts, pesa taslimu, n.k – kama ilivyo orodheshwa katika Kurasa zilizoambatanishwa.⁸
- (2) Mimi nadaiwa thamani za pesa na bidhaa, mikopo, dhamana, n.k – kama ilivyo orodheshwa katika Kurasa zilizoambatanishwa⁹.

⁸ Tumia Kurasa zipatikanazo mwishoni mwa Hati hii.

⁹ Tumia Kurasa zipatikanazo mwishoni mwa Hati hii.

KIFUNGU CHA 1V – MAAFIKIANO YA MADENI NA MATUMIZI

- (1) Mimi naamuru yakwamba mali zote za dhamana ninazomiliki zirudishwe kwa wenyewe wahusika. Na nazidi kuamuru yakwamba wakili wangu kwanza atangulize mali zangu katika kulipa madeni yangu yote halali, yakiwemo matumizi yangu yaliyotokana na ugonjwa wangu wa mwisho na mazishi yangu, na pia matumizi ya usimamizi wa mali yangu. Namuamuru aliye wakili wangu anilipie kila deni linalonipasa mimi mbele ya Mwenyezi Mungu, ikiwemo *Zakaah, nadhiri, kaffaaraat*, na ukosefu wa Hajj.
- (2) Mimi naamuru yakwamba urathi wote, mali, na kodi zitakazofuatana (zikiwemo nyongeza na malipo ya adhabu yanayotozwa), kulipwa kwa ajili ya kifo changu, zitatokamana na, na kwa ujumla zitatozwa dhidi ya, rasilmali ya mabaki ya mali bila ya malipo kutoka kwa mtu yoyote; isipokuwa ikiwa maafikiano haya hayatoleta maana kama kwamba ni yenye kuzisamehe haki zozote alizonazo wakili wangu, kisheriya au vyovyyote iwavyo, kudai malipo ya kodi zozote kama hizo zinazostahiki kulipwa katika deni la mali, kama ipo, ambayo juu yake nina mamlaka ya maagizo.

KIFUNGU CHA V – MICHANGO NA KUTUMA PESA (*HAWALA*)

- (1) Mimi nausiya juu ya vitu vifuatavyo na viwango (vyo pesa) kama wasiya wa kutuma pesa na/au upaji wa michango kwa njia ya sadaka kwa mtu aliyetajwa hapo chini na vyama.

Jina la Mtu au Chama	Kitu	Thamani
Jumla		%

- (2) Michango hii iendeleayo kukusanywa na ichukuliwe kutoka katika mabaki ya mali yangu baada ya utekelezaji wa **KIFUNGU CHA 1V**, ili itakapojuumlishwa isizidi thuluthi moja ya hayo mabaki yenyewe. Kama sivyo, kila kiwango cha michango inayoendelea

haina budi kupunguzwa kwa kadiri inayolingana ili ujumlishaji wake usizidi kiwango cha thuluthi moja.

KIFUNGU CHA V1 – UGAWAJI WA MALI YANGU NILIYOIWACHA.

- (1) Mimi natoa maagizo na kuusia yakwamba, mali yangu yote itakayo baki, baada ya utekelezaji wa **KIFUNGU CHA 1V** na **KIFUNGU CHA V**, pamoja na kiwango chochote cha mali yangu iliyokanushwa au kunyimwa na mrathi yoyote aliyetajwa jina lake au aliyehusishwa kwenye waraka huu wa wasiya, iwafikiye warathi wangu peke yao walio Waislamu ambaa uhusiano wangu mimi na wao, katika hali yoyote itokeayo, ema kwa wazazi au wazaliwa, kwenye kila hali na hatua, kuitia kwa uhusiano wa damu au ndoa halali. Ugawaji wa mali yangu iliyobaki ushughulikiwe kulingana na *Sheriya ya mirathi ya Kiislamu* halisi, kama ilivyofupishwa katika kurasa zilizoambatanishwa pamoja.
- (2) Mimi natoa maagizo na kuusia yakwamba, si ruhusa kwa jamaa yangu yoyote asiyekuwa Muislamu kurithi chochote katika ugawaji wa mali yangu iliyobaki, isipokuwa warathi waliotajwa majina yao kwenye **KIFUNGU CHA V**.
- (3) Iwapo kifo changu kitatokana na mauaji, mimi nausiya yakwamba muuaji atakaehukumiwa, ima awe ni muhusika au msaidizi kwenye mauaji yenyewe, na atapokonywa haki ya kupata urathi wowote au fungu la mali yangu.
- (4) Mimi natoa maagizo na kuusia yakwamba, hapana sehemu yoyote ya utajiri wangu itakayopewa jamaa zangu ambaa uhusiano wangu mimi na wao, wakiwa ni wazazi au wazaliwa, imetokea kwa njia ya ndoa zisizoambatana na Uislamu, mafungamano ya haramu, au mtoto wa kulelewa, isipokuwa: (a) warathi wakitajwa kwa majina kwenye **KIFUNGU CHA V**, au (b) watu wanaohusiana na mimi kwa kuitia kwa mama-mzazi. Nakariri yakwamba uhusiano wenye kuegomezwa juu ya ndoa halisi ya *Uislamu* itakubaliwa – Bila ya kujali iwapo ndoa hiyo imethibitishwa au haikuthibitishwa na mamlaka ya katiba (ya nchi).
- (5) Mimi nausiya kuhusu kiumbe chochote kilicho katika uzao wa aliyekuwa mke wangu (*kijusu*), kilichopatikana kabla ya kufa kwangu, ambacho uhusiano wake na mimi unaruhusu awe mrathi wangu kulingana na sheriya ya Uislamu, atathubutu kuwa ni mrathi wangu, maadamu atakuwa amezaliwa hai, na awemo ndani ya muda unaostahiki¹⁰ baada ya kufa kwangu. Itokeapo hali hiyo, ugawanyaji wa mali zangu nilizoziwacha baada ya utekelezaji wa **Kifungu cha 1V** na **V**, utaakhirishwa hadi baada ya mazazi ya *kijusu* hicho. Iwapo baadhi ya warathi wengine watakuwa katika hali ya matatizo ya kifedha, wanaweza kupewa kiwango cha malipo kisichozidi uchache wa fungu lao wanaloastahiki baada ya kuzingatia fungu la *kijusu*.
- (6) Mimi nausiya yakwamba mali yoyote niliyoiwacha, baada ya utekelezaji wa **Kifungu cha 1V** na **V**, na **Sehemu ya Kwanza** hadi ya **Tano ya Kifungu V1**, zihudumie katika chama kifuatacho cha ki-Islamu kisickotozwa kodi.

¹⁰ Kawaida ya “Muda unaostahiki” ni miezi tisa, lakini unatafautiana baina ya wanawake. Kwahivyo, huwenda ushauri wa utabibu ukahitajika paingiapo shaka yoyote.

KIFUNGU CHA V11

Mimi naagiza na kuusiya yakwamba iwapo sehemu yoyote ya Waraka huu wa Hati ya Urathi na Wasiya hautozingatiwa na Mahakama ya uhalalishaji wa ki-Sheriya, basi sehemu nyengine zitaendelea kuwa halali na kuweza kutumika.

UHATIMISHO

Huu ndio Wasiya wangu, ambao niliojitarishia.

فَمَنْ بَذَلَهُ وَبَعْدَمَا سَمِعَهُ، فَإِنَّمَا إِثْمُهُ عَلَى الَّذِينَ يُبَذِّلُونَهُ^{١١} إِنَّ اللَّهَ سَمِيعٌ



181. Na atakaye ubadilisha wasia baada ya kuusikia, basi dhambi yake ni juu ya wale watakao ubadilisha; hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia Mwenye kujua.¹¹

Namuomba Mwenyezi Mungu aniongoze mimi na Waislamu wote na atuja’alie tuwe mionganini mwa walio wema, mwisho mwema, na atufishe juu ya Kalimah ya kuushuhudilia Uislamu.

¹¹ Soorah al-Baqarah 2:181